# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA NNE

## KIKAO CHA KWANZA

**31 AGOSTI, 2021**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA NNE

## KIKAO CHA KWANZA – TAREHE 31 AGOSTI, 2021

**I. WIMBO WA TAIFA NA WIMBO WA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI:**

**II. DUA KUSOMWA NA KIKAO KUANZA SAA TATU ASUBUHI:**

**III. TAARIFA YA SPIKA:**

**IV. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**MWENYEKITI WA KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE:**

Taarifa ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge.

## V. MASWALI:

### OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**1. MHESHIMIWA ALLY JUMA MAKOA (KONDOA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itakarabati au kujenga Hospitali mpya ya Halmashauri ya Mji wa Kondoa kwa kuwa Hospitali iliyopo ni ya muda mrefu na miundombinu yake ni chakavu.

**2. MHESHIMIWA BAHATI KENETH NDINGO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itakamilisha uanzishwaji wa Hati Fungani za Serikali ya Mitaa.

### OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):

**3. MHESHIMIWA DENNIS LAZARO LONDO (MIKUMI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

(a) Je, ni Watumishi wangapi wamerejeshwa kazini baada ya kuondolewa kimakosa wakati wa zoezi la uhakiki wa vyeti feki na Wafanyakazi hewa;

(b) Je, ni Watumishi wangapi waliorejeshwa kazini wamelipwa stahiki zao ambazo hawakulipwa kutokana na kuondolewa kazini.

**WIZARA YA KILIMO:**

**4. MHESHIMIWA ANTHONY PETER MAVUNDE (DODOMA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuliendeleza zao la Zabibu Mkoani Dodoma.

**5. MHESHIMIWA YUSTINA ARCADIUS RAHHI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua changamoto ya upatikanaji wa huduma za Ugani Mkoani Manyara zinazotokana na upungufu wa Wataalam wa Kilimo na Mifugo katika ngazi ya Kata na Vijiji.

**WIZARA YA MAJI:**

**6. MHESHIMIWA ALEXANDER PASTORY MNYETI (MISUNGWI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:- Chanzo cha Maji cha Ihelele kilichopo Kijiji cha Nyanhomango kinasambaza maji katika Mikoa ya Shinyanga na Tabora:-

Je, ni lini Serikali itapeleka miundombinu ya maji kwenye Kijiji hicho pamoja na Vijiji vingine vinavyozunguka chanzo hicho.

**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:**

**7. MHESHIMIWA KAVEJURU ELIADORY FELIX (BUHIGWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itajenga *Standard Gauge Railways* kutoka Tabora kwenda Kigoma.

**WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**

**8. MHESHIMIWA MWANTATU MBARAK KHAMIS (BLW):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwainua Watu Wenye Ulemavu kwa kuwapatia vifaa vya michezo na Walimu ili waweze kushiriki mashindano ya kitaifa na kimataifa.

## WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

**9. MHESHIMIWA SAADA MANSOUR HUSSEIN (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, ni lini Serikali itawapatia Vitambulisho vya Taifa Wananchi wote waliojiandikisha.

## WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:

**10. MHESHIMIWA MARIAM MADALU NYOKA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuifanyia ukarabati mkubwa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Ruvuma kwa kuwa ni ya muda mrefu na majengo yake yamechakaa.

**WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

**11. MHESHIMIWA MOHAMMED MAULID ALI (KIEMBE SAMAKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa:-

(a) Je, Serikali inatambua mgogoro wa ardhi uliopo baina ya Wananchi na Kambi ya Jeshi la Wananchi iliyopo Chukwani Zanzibar;

(b) Je, Waziri yupo tayari kufuatana na Mbunge ili kukutana na Wananchi na kufahamu hali halisi ya mgogoro huo uliodumu kwa muda mrefu.

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

**12. MHESHIMIWA BRYCESON MAGESSA TUMAINI (BUSANDA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

Je, Serikali imejipangaje katika kupanga matumizi bora ya ardhi kwa Vijiji vyote nchi nzima ili kuondokana na migogoro ya matumizi ya ardhi.

## WIZARA YA NISHATI:

### 13. MHESHIMIWA ZUENA ATHUMANI BUSHIRI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kusambaza umeme katika Vijiji na Vitongoji kupitia REA III hasa katika maeneo ambayo nguzo zimetelekezwa barabarani zaidi ya miaka miwili.

## WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

### 14. MHESHIMIWA DANIEL AWACK TLEMAI (KARATU):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua mgogoro wa mpaka kati ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro na Kata ya Mbulumbulu katika Kijiji cha Lositete.

## VI. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

***(Kusomwa Mara ya Kwanza)***

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mwaka 2021 *[The Fire and Rescue Forces (Amendment) Bill, 2021]*

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.5) wa Mwaka 2021 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 5) Bill, 2021]*

## VII. HOJA ZA KAMATI:

**MWENYEKITI WA KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE:**

Taarifa ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge.

**DODOMA** **N.J. MWIHAMBI, *ndc***
**31 AGOSTI, 2021** **KATIBU WA BUNGE**

PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA